

**TARGETER WINGS**  
**KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI**



**GREDI 5 - 2022**



**SHUGHULI ZA KISWAHILI**

**Muda: Saa 1**

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali**



- Daktari** : Hujambo?  
**Mgonjwa** : Sijambo daktari ila naumwa na kichwa.  
**Daktari** : Ulianza kuumwa lini?  
**Mgonjwa** : Juzi jioni.  
**Daktari** : Unaugua mahali pengine?  
**Mgonjwa** : Ndio, pia tumbo linanisokota.  
**Daktari** : Pole utapona.  
**Mgonjwa** : Nashukuru  
**Daktari** : Naomba nikupime joto la mwili. Tafadhali vua koti nikupime. (Baada ya muda mfupi) Naona joto liko juu kidogo. Dawa nitakazokupatia zitakusaidia.  
**Mgonjwa** : Asante daktari

1. Mazungumzo yalikuwa kati ya watu wangapi?  
A. Watatu                      B. Wawili                      C. Watano                      D. Mmoja
2. Ni nani aliyeamkua mwingine?  
A. Mgonjwa                      B. Mwuguzi                      C. Daktari                      D. Mtoto

3. Mgonjwa alipopimwa joto, matokeo yalikuwa yapi?
  - A. Joto lilikuwa hali ya kawaida
  - B. Hakuwa na joto
  - C. Joto lilikuwa juu zaidi
  - D. Joto lilikuwa juu kidogo
4. Daktari alitaka kujua nini kutoka kwa mgonjwa?
  - A. Alianza kuumwa lini?
  - B. Ametumia dawa zipi?
  - C. Maumivu ya koo
  - D. Kuumwa sana
5. Ni nani aliyeambia mwingine pole?
  - A. Mzazi
  - B. Ni mgonjwa
  - C. Ni daktari
  - D. Ni wote

**Soma kifungu kifuatacho cha shairi kisha ujibu maswali 6-10**

Mtaka cha mvunguni, hana budi kuinama,  
 Nanyi humu darasani, hamna budi kusoma,  
 Tumeambiwa shuleni, na pia baba na mama,  
 Kwamba juhudi ni pato, kufaulu jitihadi.

6. Walio darasani hawana budi \_\_\_\_\_
  - A. kusoma
  - B. kuvunguni
  - C. kuchapa kazi
  - D. kutii
7. Kati ya haya maneno ni lipi halijatajwa?
  - A. Baba
  - B. Shuleni
  - C. Shangazi
  - D. Mama
8. Ili kufaulu unafaa kufanya nini?
  - A. Kucheza
  - B. Kuiga
  - C. Kujitahidi
  - D. Kutofaulu
9. Methali mtaka cha mvunguni, hana budi kuinama humaanisha nini?
  - A. Unafaa kutia bidii
  - B. Usifuatae wenzako
  - C. Usiingie mvunguni
  - D. Usihangaika
10. Neno shuleni lina silabi ngapi?
  - A. Nne
  - B. Tano
  - C. Tatu
  - D. Tano

**Soma ufahamu kisha ujibu maswali 11-13**

Tumbiri na Binadamu walikuwa ndugu wa kufa kuzikana. Waliishi pamoja wakisaidiana kazi za nyumbani. Wote walikuwa na ngozi laini na nyororo. Siku moja Tumbiri na Binadamu walitayarisha maharagwe na kuyaweka kwenye sufuria. Waliwasha jiko na kuwika sufuria ya maharagwe juu yake.

Kama ilivyokuwa mazoea yao, Tumbiri na Binadamu walienda kuoga mtoni. Tumbiri alijisugua kichwani na mwili wote. Binadamu pia alifanya vivyo hivyo huku maharagwe yakiendelea kuiva.

Hatimaye, Tumbiri na Binadamu walienda nyumbani. walijipakulia maharagwe yaliyoiva. Kila mmoja akapata kiasi sawa na mwengine. Tumbiri alikula sehemu yake. Binadamu akala yake. Hata hivyo Tumbiri hakushiba. Tumbiri alitamani kujiongezea mlo. Hivyo, alitafuta njama ya kujiongezea chakula.

11. Nani walikuwa ndugu wa kufa kuzikana?  
 A. Wanyama wa pori  
 B. Tumbiri na simba  
 C. Binadamu na Tumbiri  
 D. Wanyama wanaoisha kwenye maji
12. Ndugu wa kufa kuzikana inamaanisha nini?  
 A. Kupendana sana  
 B. Wanaofanana sana  
 C. Kukaribiana sana  
 D. Majirani wa karibu
13. Kati ya hawa wawili ni yupi hakushiba?  
 A. Simba  
 B. Nyoka  
 C. Tumbiri  
 D. Binadamu

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 14-15.**

Baba alipokata kauli kupunguza shughuli aliendelea kuwa na afya nzuri. Tuliendelea kuzungumza naye mambo aliyofurahia kusikiliza kama vile umilisi tuliokuwa tumepata shuleni. Haswa, alifurahi tulipomwambia tuliyojifunza kuhusu jinisi ya kuzuia magonjwa yanayotokana na hali za maisha kama vile kisukari na shinikizo la damu.

14. Ni nini maana ya kukata kauli?  
 A. Kupenda  
 B. Kuamua  
 C. Kuelezea  
 D. Kusoma
15. Jambo lipi haswa lilimfurahisha Baba?  
 A. Hadithi za kale  
 B. Masomo ya sayansi  
 C. Jinsi ya kuzuia magonjwa  
 D. Hali za maisha

**Soma kifungu kifuatacho. Kwa kila swali umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaale zaidi kati ya yale umepewa.**

Baba Ali aliendeleza biashara yake 16 kufungua duka 17 jumla. Aliwaajiri wafanyikazi zaidi. Walikuwa waaminifu na wenye 18 kazini. Wafanyikazi 19 waliendeleza kupitia mishahara 20.

16. A. na  
 B. wa  
 C. vya  
 D. kwa
17. A. ya  
 B. la  
 C. cha  
 D. za
18. A. bidii  
 B. uzembe  
 C. mchezo  
 D. ulaghai
19. A. yao  
 B. zao  
 C. yake  
 D. wake
20. A. walizopokea  
 B. waliopokea  
 C. waliyopokea  
 D. waliupokea

**Swali la 21 hadi la 30, chagua jibu sahihi.**

21. Jibu la safari njema ni \_\_\_\_\_  
 A. pia nawe  
 B. sawa  
 C. aha  
 D. asante

